

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa,
148 Br. ya Kayenze,
33383 Nyehunge,
SENGEREMA, MWANZA.

01 Machi, 2024

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MUDA WA MIEZI MITATU YA
WAKUSANYA MAPATO (REVENUE COLLECTORS)**

Ninayo furaha kutangaza nafasi ishirini (20) za kazi ya Mkataba ya ukusanyaji mapato (revenue collectors) ambao wataajiriwa kwa muda wa miezi mitatu kuanzia tarehe 1, Aprili, 2024 hadi tarehe 30, June 2024. Mapato hayo yatakusanywa katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama vitakavyoonekana kwenye Mkataba.

MAJUKUMU YA KAZI:

1. kukusanya mapato toka kwenye vyanzo vya mapato atakayopangiwa
2. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yaliyokusanywa kwa siku hiyo yanawekwa Benki
3. Kuhakikisha kuwa makusanyo yote yanakusanywa kwa kutumia mashine ya kukusanyia mapato (POS MACHINE) na kutoa stakabadhi halali za Halmashauri
4. Kuhakikisha kuwa mashine ya kukusanyia mapato (POS MACHINE) inakuwa katika hali nzuri na inatumika muda wote bila kuzimwa
5. Kufanya kazi yoyote utakayopangiwa na msimamizi wa kazi

MALIPO

Malipo kwa kazi hii ni asilimia 10 (10%) ya makusanyo atakayokusanya katika chanzo husika kwa kila mwezi.


SIFA MUHIMU ZA WAOMBAJI:

1. Awe raia wa Tanzania ambaye ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya Buchosa.
2. Awe amesajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania (TIN)
3. Awe na kitambulisho vya Taifa (NIDA)
4. Awe amehitimu kidato cha Nne au cha sita
5. Awe na umri wa Miaka 18 hadi 45
6. Awe na ujuzi wa kutumia kwa ufasaha simu janja (smart phone)
7. Mwombaji anatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika katika maeneo wanakotoka.
8. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha picha mbili (pass port size) za rangi za hivi karibuni.
9. Awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha Lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
10. Awe mwaminifu, mwadilifu, na mwenye weledi.
11. Awe hajawahi kupatikana na hatia kwa makosa ya jinai.
12. Mwombaji akatakayekidhi sifa zinazotakiwa ataajiriwa na kupangwa kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya mapato vya Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa.
13. Mwombaji awe hadaiwi na Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa au Halmashauri yoyote ambayo amewahi fanya kazi ya kukusanya mapato
14. Barua ya maombi ipitie kwa Mtendaji wa Kijiji au Kata
15. Barua ya maombi iwe na namba za simu na anuani ya kuaminika
16. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na viambatanisho vinavyohitajika kama vile nakala ya Cheti cha mlipa kodi (TIN) ,Cheti cha kidato cha nne au Kidato cha sita, NIDA Namba na zitumwe kwa Anwani ifuatayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,
HALMSHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA,
S. L. P. 44,
BUCHOSA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe **14 Machi, 2024** saa 9.30 Alasiri

IMETOLEWA NA MKURUGENZI WA HALMSHAURI YA BUCHOSA



**Benson P. Mihayo
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA**

NAKALA:

- ✓ Mbao zote za matangazo Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa